

**KUMB. NA. BSS/JI/2021 N/VOL.18**

Jina la mwanafunzi.....

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI BUSHASHI**

**1. UTANGULIZI**

Nafurahi kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza 2021 katika shule ya Sekondari ya Bushashi. Mhula wa masomo utaanza 11/01/2021 na unatakiwa kuripoti shule 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni 25/01/2021.

**2. Mambo ya kuzingatia**

**2.1 SARE ZA SHULE**

(a) Suruali nyeusi 2 ( kitambaa namba moja) kwa wavulana zenye marinda mawili na mifuko matatu  
(3). Sketi 2 nyeusi (kitambaa namba moja) kwa wasichana zenye marinda, sketi iwe ndefu kuvuka magoti.

(a)Shati /blauzi 2 zenye mikono mifupi.(TOMATO)

(C) Viatu vyeusi vyenye visigino vifupi na vyenye kamba, Soksi nyeusi kwa wavulana na nyeupe ndefu kwa wasichana.

(d) T-shirt rangi ya damu ya mzee yenye (mhuri) nembo ya shule kwa kazi za nje na michezo.

**2.2 VIFAA VYA KUJIFUNZIA**

Daftari tisa (9) counter book (3Q), kalamu, mkebe wa hesabu(Mathematical sets) na kamusi (Dictionary) ya kingereza ya kujifunzia.

**3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu NA. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebisha kwa sheria na. 10 ya mwaka 1995. Kwa hiyo unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo baada ya kuripoti shuleni;

(a)Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingna na ratiba ya shule ni jambo la lazima.

(c) Kushirikiana kwa makini kufanya maandalio ya jioni(preparation)

- (d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na zingine utakazopewa.
- (e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- (f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
- (g) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
- (h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
- (i) Kutunza mali ya shule.

**4. Makosa yafuatayo yanaweza kukusababisha kufukuzwa shule/Kusimamishwa masomo;**


- (a) Wizi
- (b) Uasherati
- (c) Ubakaji
- (d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k
- (e) Kupigana
- (f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- (g) Kudharau Bendera ya Taifa.
- (h) Kupata mimba/kumpa mimba mwanafunzi.
- (j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- (i) Kukataa adhabu kwa makusudi.
- (i) Kumiliki simu ya mkononi au laini ya simu.

**5. Mambo mengine Muhimu yanayopaswa kukamilishwa shuleni na mwanafunzi.**

- (a) kujaza fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi.
- (b) kujaza fomu ya Mzazi kukiri kukubaliana na sheria na kanuni za shule.
- (c) Kuja na cheti cha kuzaliwa/kadi ya kliniki.
- (d) kuja na fomu ya kupima afya iliyosainiwa na mganga.

NB.Fika na fomu zote zikiwa zimejazwa kikamilifu wakati wa kuripoti

Karibu sana



ROBERT J. BALELE

MKUU WA SHULE.

**THE HEADMASTER  
BUSHASHI SECONDARY SCHOOL  
MASWA**